

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**MHE.PAUL MAKONDA AMEWEKA JIWE LA MSINGI KATIKA JENGO LA DHARURA
HOSPITALI YA TEMEKE**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa Paul C. Makonda leo ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la kisasa la huduma za dharura (EMERGENCY BLOCK) Hospitali ya Temeke ambalo ujenzi wake utagharimu zaidi ya shilingi Million 800 linalofadhiliwa na ubalozi wa Japan Nchini Tanzania.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Mheshimiwa Makonda amesema jengo hilo litakuwa na uwezo wa kusaidia zaidi ya watu 2000 kwa siku ambapo litakuwa na chumba cha upasuaji, chumba cha ICU, vyumba vya uangalizi maalumu wa wagonjwa pamoja na vyumba vya madaktari.

Aidha jengo hilo litakuwa na vyumba maalumu vya watoto (njiti), Kinamama na Wababa ambapo lengo ni kuhakikisha **Mgonjwa yoyote wa Dharura** iwe wa Ajali, Upasuaji kwa kinamama Wajawaziito, Malaria ya ghafla, Moto na wanaobanwa na Kifua wanapatiwa huduma ya haraka ambapo kwa hatua hiyo itasaidia kupunguza mlundikano wa Wagonjwa wa dharura Hospital ya Taifa Muhimbili kama Rais Dkt.Magufuli anavyotaka.

“Mimi nimeshuhudia watu wengi wakipoteza maisha kwa kukosa huduma za dharura, hii ndio iliyonisukuma kutafuta kila njia ili wananchi wangu wasipoteze maisha kwa sababu tu ya kukosa huduma ya haraka, nikaamua kumtafuta balozi wa Japani na kumshirikisha jambao hili, Balozi aliponisikiliza na kunielewa akakubali kuniunga mkono katika mapambano yangu ya kuboresha huduma za afya kwa wananchi hasa

wanyonge na ameshanipa fedha kwaajili ya ujenzi wa jengo hilo na hivi tunavyoongea tayari mkandarasi ameanza na ujenzi” Alisema Makonda.

Aidha Mheshimiwa Makonda amesema kuwa ujenzi wa jengo hilo utachukuwa miezi sita hadi kukamilika na kueleza kuwa dhamira yake ni kuhakikisha Dar es salaam inakuwa Mkoa unaotoa huduma bora za Afya.

“Watu hatukumbukwi kwa maneno bali kazi tulizofanya. Kwa kuwa Rais Magufuli amenipa Mkoa niongoze na mimi ni lazima nitumie akili na kipaji ambacho Mungu amenipa kutatua Changamoto za Afya katika Mkoa wangu” Aliongeza Makonda.

Kwa upande Mwakilishi wa Balozi wa Japani Nchini Tanzania Bwana Hiroyuki Kubota amesema serikali ya Japan itaendelea kushirikiana na Tanzania katika masuala mbalimbali huku Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mheshimiwa Felix Lyaniva akimpongeza Makonda kwa namna anavyopambana kutatua kero za Wananchi.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

11/07/2017